

SOMO LA IMANI:

Maandiko: EBR.11:1

1. UTANGULIZI

Imani kwa mujibu wa **Biblia** ina sifa (tabia) **5 kuu; (Imani ni kuwa na hakika na ni bayana ya vitu visivyoonekana.**

- a. **Math. 8: 5 – 13. Imani inapimwa na Bwana kama ni kubwa ama ndogo tofauti na wokovu ambao hakuna anayeweza kuupima ili kujua kuwa huyu ameokoka zaidi kuliko yule. Soma pia Math. 15: 21 - 28.**

Siri ya imani kuwa kubwa ni pale mtu anapovumilia bila kulalamika wakati anapokuwa anapita katika dhiki na majaribu na kubakia mwaminifu kwa Yesu hata kama inaelekea kama Mungu hatajibu hitaji lake au kujali shida yake. **Luk. 18: 1-7 (Hii wakati mwingine huitwa imani inayong'oa milima. Mark. 11: 20 – 24.**

- b. **Imani tabia yake ya pili** huwa kuna wakati **inajaa** na kuna wakati **inapungua/inatindika. Luk. 22: 31- 32, Mdo. 6:5, Math. 14: 26 – 31.** Kama Yesu alivyomwomba Petro ili imani yake isitindike, haya ndiyo maombi ya Roho Mtakatifu kwetu kwamba imani yetu iwe imejaa wakati wote hata tunapokabiliana na dhoruba; ikitindika tu shetani anatufunga goli.

c. Imani nayo ina chakula chake maalumu kabisa inachokipenda ambacho ni shida na majaribu.

Esta 4: 14 – 17, 5: 1 – 5; Mwz. 45: 1 – 15. Kama hakuna jambo gumu unalokabiliana nalo imani inakuwa haina kazi. **1Samwl. 17: 31 – 54.**

- Imani ni kama **tochi** ambayo haina kazi kama hakuna giza-faida ya tochi unaiona wakati wa giza nene. **Kut.14: 9 – 14, 2Wafal. 7: 3 – 14.**

d. Imani ina tabia ya kutotaka mjadala; bali yenyewe inasimama na Neno la Mungu tu. Math. 14: 25 – 29, Yoh. 2: 2 – 11*(5), Mark. 9: 14 - 29, Ebr. 11: 8 – 11 (Iko kinyume kabisa na akili za wanadamu; pale wanaposema **haiwezekani**, imani inaona **uwezekano, hapana** njia, imani **inaona** njia n.k.

e. Imani inaweza kuwa dhaifu au kuwa imara; Rumi 4: 19 – 20, 14: 1 -2; (hujawahi kuona mtu mwingine ana imani ya kuponywa ugonjwa lakini hana imani ya kujenga nyumba nzuri au kuwa tajiri, au kununua gari zuri n.k. ndiyo sababu Paulo anawaandikia Warumi hivi maana walikuwepo walio na imani ya kula vyote na wengine kula mboga za majani tu!!!

Na

Askofu Dr. L. M. Mwizarubi.

June 2021.